

WILAYA YA SHULE YA PHILADELPHIA
OFISI YA MIPANGO ISIYO YA UMMA
440 N. Broad Street 3rd Floor Portal D
Philadelphia, PA 19130
Karla Wargo, Mkurugenzi.
Nambari ya Simu: 215-400-6032
Nambari ya Faksi: 215-400-4224

Mpendwa Mzazi/Mlezi,

Barua hii ni kukufahamisha kwamba mtoto wako atakuwa anapokea msaada na usaidizi wa kimafundisho kutoka kwa mpango wa Title I unaofadhiliwa na serikali ya shirikisho ulio chini ya Sheria ya 2001 ya Hakuna Mtoto Ataachwa Nyuma katika mwaka wa shule wa 2016/2017. Mtoto wako ametambuliwa kupokea huduma hii kulingana na vigezo vya ustahiki vilivyowekewa darasa la mtoto wako. Mafundisho yatatekelezwa shuleni mwa mtoto wako na mfanyikazi mwenye uhitimu wa juu katika mafundisho ya Title I. Huduma zitatolewa katika siku za kawaida za shule au kupitia mpango wa muda wa ziada. Mtoto wako atakuwa anashiriki katika mpango ufuatao isipokuwa uamue vinginevyo:

- | | |
|---|---|
| <input type="checkbox"/> Masomo ya Lugha ya Kiingereza | <input type="checkbox"/> Uboreshaji Hisabati |
| <input type="checkbox"/> Mpango wa Muda wa Ziada – Ruhusa Inahitajika | <input type="checkbox"/> Uboreshaji ujuzi wa Kusoma |

Sheria ya 2001 ya Hakuna Mtoto Ataachwa Nyuma ndio msaada mkubwa zaidi nchini wa serikali ya shirikisho. Ufadhili huu wa Title I unatuwezesha kusaidia mpango wa elimu ya kawaida wa mtoto wako kwa kutoa mafundisho ya ziada kwa wanafunzi katika stadi msingi za kusoma na hisabati na vile vile katika Lugha ya Kiingereza.

Tunatazamia kushirikiana nawe, mwalimu mkuu wa shule wa mtoto wako na mwalimu wake wa elimu ya kawaida katika kutoa mpango wa usaidizi wa kielimu kwa mtoto wako. Ili kupata taarifa za ziada kuhusiana na ushiriki wa mtoto wako katika mpango wa Title I, tafadhali wasiliana na mwalimu wa Title I wa mtoto wako.

Karla Wargo, Mkurugenzi
Mipango Isiyo ya Umma

Nk: Thomas Smith, Independence Mission Schools
Walimu Wakuu wa Shule za Kibinafsi
Mwalimu wa Elimu ya Kawaida

BARAZA LA USHAURI KWA MZAZI LA TITLE I
KITENGO CHA MIPANGO YA SHIRIKISHO PDE

WILAYA YA SHULE YA PHILADELPHIA
KIFURUSHI CHA MZAZI CHA MPANGO USIO WA UMMA WA TITLE I

Mpango wa Title I Usio wa Umma wa Wilaya ya Shule ya Philadelphia utatoa mtaala na mafundisho ya ubora wa juu katika mazingira ya usaidizi na fanisi ya mafunzo ambayo yatawezesha mafanikio kwa kila mwanafunzi na:

- 1.) Utafunza kila mtoto kwa hadhi na heshima.
- 2.) Utajitahidi kuangazia mahitaji binafsi ya kila mwanafunzi.
- 3.) Unatambua kwamba wazazi ni wa muhimu katika mafanikio ya shule hii na wanafunzi wake.
- 4.) Utatoa mazingira salama, chanya na mazuri kwa mafunzo kwa kila mwanafunzi.
- 5.) Utahakikishia kila mwanafunzi kupata mafunzo mazuri ambayo ni mwafaka mwa maendeleo yake.
- 6.) Utahakikisha kwamba wafanyikazi wa shule wanatoa mawasiliano kuhusu matarajio wazi ya matokeo kwa wanafunzi na wazazi.
- 7.) Utahakikishia ushiriki mwafaka wa wazazi katika kufanya maamuzi yanayohusiana na elimu ya watoto wao.